

LUGHA YA KISWAHILI KATIKA TAMASHA ZA DRAMA NCHINI KENYA: KUSTAWI AU KUDUMAA?

Francis G Waititu

Chuo Kikuu cha Moi, Eldoret

Ikisiri

Tamasha za drama ambazo hufanywa kila mwaka nchini Kenya ni mojawapo ya nyenzo zilizowekwa na wizara ya Elimu nchini kutoa elimu kwa vijana. Tamasha hizi ambazo zinajumuisha wanafuzi kutoka shule za malezi, msingi, sekondari, vyuo anuai na vyuo vikuu hufanyika kila mwaka. Tamasha huanzia mashinani na kilele huwa kujumuika kwa timu ambazo zimeshinda katika ngazi mbalimbali kwa mashindano ya kitaifa ambayo aghalabu hufanyika mwezi wa Aprili. Mojawapo ya malengo ya tamasha hizi ni ustawishaji wa lugha za Wakenya miongoni mwa wanaoshiriki. Tangu mbalimbali kama michezo ya kuigiza, ngoma, mashairi, sarakasi na masimulizi huwasilishwa. Washiriki huwa na uhuru wa kuwasilisha chochote wanachokiwasilisha kwa lugha yoyote kuanzia Kiswahili, Kiingereza na lugha nyingine za Kenya. Hata hivyo, imebainika kuwa kazi nyingi ambazo hupata matuzo ni kazi katika lugha ya Kingereza. Makala hii inalenga kuchunguza kiwango cha matumizi ya lugha ya Kiswahili katika tangu zinazowasilishwa hasa katika ngazi ya kitaifa. Makala itachunguza tangu zinazowasilishwa kwa lugha ya Kiswahili huku ikilinganisha zinazowasilishwa kwa lugha ya nyingine ili kubainisha ni kwa nini tangu kwa lugha ya Kiswahili hazifikii kupata matuzo. Aidha, makala itachunguza iwapo katika tamasha hizi, Kiswahili hupata nafasi ya kustawi au kudumaa.